Jarida La

# MIFUGO NA UVUVI

#mifugonauvuviniutajiri

TOLEO NO; WMUV 0004| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

Yaliyojiri Mwezi Aprili 2025



## Serikali yaja na Njia Mpya Kudhibiti Uvuvi Haramu Ziwa Victoria

- *Ni Ndege Nyuki 'Drone' itakayofanya doria hadi Saa Mbili Angani*



**Prof. Shemdoe abainisha Fursa za Malisho**



**Serikali Kuwezesha Ufugaji wa Kisasa**

*Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu*

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni HALIUZWI

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Yaliyomo *Ndani* Jarida


1 TAHARIRI .............**Uk. 04**

2 Ndege Nyuki ' Drone' yaanza kuwasaka Wavuvi Haramu Ziwa Victoria .......**Uk. 05 - 06**

3 Mifugo Zaidi ya Milioni 370 yapatiwa Chanjo dhidi ya Magonjwa .......**UK 07**

4 Meli ya Utafiti wa Uvuvi wa Baharini yapokelewa Zanzibar ............. **Uk. 08**

5 Kongamano la Nguruwe Afrika kufanyika Nchini Tanzania ........... **Uk. 09**

6 Matukio katika picha ya uzinduzi wa Ndege Nyuki 'Drone' uliofanywa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti Jijini Mwanza.... **Uk. 10**

7 Prof. Shemdoe abainisha fursa za Malisho ya Mifugo...... **UK. 11**

8 Wavuvi, Wachuuzi wa Samaki kutumia mfumo wa 'Vua, Uza na Nunua Kidigitali' ........... **Uk. 12**

9 Wafugaji Nchini wahimizwa kulima Malisho ya Mifugo ............ **Uk. 13**

10 TDB yahimizwa kuendelea kuwasajili wadau wa Tasnia ya Maziwa............ **Uk. 14**

11 Serikali Kuendelea kuwezesha Ufugaji wa Kisasa ....... **Uk. 15**

12 Serikali yakabidhi Gari la Ubaridi kwa Chama cha Ushirika wa Uvuvi BUKASIGA Ltd......**Uk. 16**

13 Matukio katika Picha ya Shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Viongozi, Wataalam na Wadau ...... **Uk.17 - 20**
















# TAHARIRI

Ziwa Victoria ni kubwa zaidi barani Afrika na la pili kwa ukubwa duniani kwa maji ya ndani, ambapo limekuwa rasilimali muhimu sana kwa Tanzania katika Sekta ya Uvuvi, kwa kuwa ziwa hili linawanufaisha zaidi ya wananchi milioni nne kwa kutoa ajira, lishe, biashara na mapato kwa serikali.

Hata hivyo, changamoto kubwa inayoendelea kulikumba ni vitendo vya uvuvi haramu, ambapo kwa miaka mingi vimekuwa vikitishia uhai wa samaki, kupunguza uzalishaji na kuharibu mfumo wa ikolojia ya maji.

Hivyo, serikali imekuwa ikichukua hatua na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na uvuvi haramu. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya maboresho ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia rasilimali za uvuvi ikiwemo matumizi ya teknolojia za kisasa katika kusimamia rasilimali za uvuvi, kuimarisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs), kutoa elimu ya kudhibiti uvuvi haramu na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa Wavuvi na kuimarisha ufugaji wa viumbe maji.

Aprili 13, 2025 Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Mifugo na uvuvi kwa mara ya kwanza imenunua na kuzindua matumizi ya ndege nyuki (drone) itakayofanya kazi ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Serikali imeamua kuchukua hatua madhubuti za kisasa kuhakikisha inadhibiti uvuvi haramu kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambapo kwa awamu hii ya kwanza Shilingi Milioni 259 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki, kutoa mafunzo kwa waendeshaji, kufunga vituo vya kudhibiti, kufanya usajili na kuanzisha mfumo wa kuhifadhi na kuchambua taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ndege hiyo.

Ndege nyuki hii ni kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria na ina uwezo wa kukimbia kwa mwendo kasi wa Kilometa 108 kwa saa na uwezo wa kuchukua picha za matukio kutoka umbali wa mita 350 na kuruka mita 120 kutoka usawa wa bahari na kusafiri umbali wa Kilometa 400 na kuweza kukaa angani kwa muda wa saa mbili.

Mpango wa matumizi ya ndege nyuki hautaishia Ziwa Victoria pekee, bali kupeleka matumizi hayo katika Ziwa Tanganyika na Nyasa, pamoja na maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi ili kuhakikisha kila pembe ya nchi inaonja matunda ya teknolojia ya kisasa katika usimamizi wa rasilimali.

Ndege nyuki hiyo ina uwezo wa kutoa taarifa kulingana na muda halisia na kwamba itasaidia kupunguza vitendo vya uvuvi haramu na gharama za uendeshaji wa doria ziwani pamoja na kutumika katika masuala ya utafutaji na uokoaji.

Ndege nyuki hiyo ni kifaa cha kisasa kinachoruka angani bila rubani kwa lengo la kusaidia kuimarisha doria na usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kuwa kifaa hicho ni mali ya serikali, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na taasisi zingine za serikali kuimarisha ulinzi na usalama kwenye Ziwa Victoria.

Katika mapambano ya uvuvi haramu serikali ililazimika kutumia boti na magari yanayotumia mafuta ya diesel ambayo yanaleta hewa ya ukaa kwa kiasi kikubwa ila kwa matumizi ya ndege nyuki, itakuwa ikienda eneo mahsusi ambalo kuna viashiria vya uvuvi haramu hivyo kupunguza matumizi ya boti na magari kwa ajili ya kuwasaka wavuvi haramu.

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka wazi kuwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki zaidi ili kuongeza wigo wa kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali nchini.

Bodi ya Wahariri inapongeza jitihada za serikali kwa kufikia hatua muhimu ya matumizi ya teknolojia za kisasa ambazo zitasaidia kulinda rasilimali za nchi na hakika zikitumiwa vyema zitaleta tija katika maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini.

**Bodi ya Wahariri:**

**Mwenyekiti**
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mhariri**
**Edward Kondela** - Afisa Habari Mwandamizi

**Msanifu**
**Hamis Hussein** - Afisa Habari

**Wajumbe**
**Elibariki Mafole** - Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike** - Afisa Habari
**Stanlay Bryaton** - Afisa Habari
**Chiku Makwai**- Afisa Habari



# Ndege Nyuki 'Drone' yaanza rasmi kuwasaka Wavuvi Haramu Ziwa Victoria

Hatua ya Serikali kudhibiti uvuvi haramu, mpango huo kutumika kwenye maziwa yote nchini.

**Na, Edward Kondela – WMUV, Mwanza**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mara ya kwanza imenunua na kuzindua matumizi ya ndege nyuki (drone) itakayofanya kazi ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ndege nyuki hiyo jijini Mwanza Aprili 13, 2025 kwa niaba ya Mgeni Rasmi Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri Mhe. Alexander Mnyeti alisema serikali imeamua kuchukua hatua madhubuti za kisasa kuhakikisha inadhibiti uvuvi haramu kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mhe. Mnyeti aliongeza kuwa katika awamu hii wizara imetumia kiasi cha Shilingi Milioni 259, kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki, kutoa mafunzo kwa waendeshaji, kufunga vituo vya kudhibiti, kufanya usajili na kuanzisha mfumo wa kuhifadhi na kuchambua taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ndege hiyo.

"Ndege nyuki hii ni kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria. Ndege nyuki hii ina uwezo wa kukimbia kwa mwendo kasi wa Kilometa 108 kwa saa na uwezo wa kuchukua picha za matukio kutoka umbali wa mita 350 na kuruka mita 120 kutoka usawa wa bahari na kusafiri umbali wa Kilometa 400 na kuweza kukaa angani kwa muda wa saa mbili." amesema Mhe. Mnyeti.

Aidha, amesema mpango wa matumizi ya ndege nyuki hautaishia Ziwa Victoria pekee, bali kupeleka matumizi hayo katika Ziwa Tanganyika na Nyasa pamoja na maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi ili kuhakikisha kila pembe ya nchi inaonja matunda ya teknolojia ya kisasa katika usimamizi wa rasilimali.

Pia, alisema ndege nyuki hiyo ina uwezo wa kutoa taarifa kulingana na muda halisia na kwamba itasaidia kupunguza vitendo vya uvuvi haramu na gharama za uendeshaji wa doria ziwani pamoja na kutumika katika masuala ya utafutaji na uokoaji.

Alifafanua kuwa ndege nyuki hiyo ni kifaa cha kisasa kinachoruka angani bila rubani kwa lengo la kusaidia kuimarisha doria na usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kuwa kifaa hicho ni mali ya serikali, wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na taasisi zingine za serikali kuimarisha ulinzi na usalama kwenye Ziwa Victoria.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede akizungumza katika hafla hiyo alisema uwepo wa ndege nyuki unaenda sambamba na takwa la kidunia

la matumizi ya teknolojia rafiki za kimazingira.

Aliongeza kuwa katika mapambano ya uvuvi haramu serikali ililazimika kutumia boti na magari yanayotumia mafuta ya diesel ambayo yanaleta hewa ya ukaa kwa kiasi kikubwa ila kwa matumizi ya ndege nyuki, itakuwa ikienda eneo mahsusi ambalo kuna viashiria vya uvuvi haramu hivyo kupunguza matumizi ya boti na magari kwa ajili ya kuwasaka wavuvi haramu.

Kufuatia maelekezo ya Naibu Waziri Mhe. Mnyeti, katika kudhibiti uvuvi haramu Dkt. Mhede alibainisha kuwa atahakikisha anasimamia maelekezo hayo yakiwemo ya baadhi ya maafisa uvuvi kutuhumiwa kushiriki katika matukio ya uvuvi haramu.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi alisema mkoa huo unategemea sana Sekta ya Uvuvi katika kukuza uchumi, hivyo kuzinduliwa kwa ndege nyuki kwa matumizi ya kudhibiti upotevu wa rasilimali za uvuvi kutasaidia kuwabaini wahalifu na kukomesha uvuvi haramu.



Alisema kama mkoa wamekuwa wakihakikisha doria zinafanyika mara kwa mara ili kuhakikisha maeneo yote ya Ziwa Victoria katika Mkoa wa Mwanza yanakuwa salama dhidi ya uvuvi haramu.

> **"** ***Ndege nyuki hii ni kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria, ina uwezo wa kukimbia kwa mwendo kasi wa Kilometa 108 kwa saa, kuchukua picha za matukio kutoka umbali wa mita 350 na kuruka mita 120 kutoka usawa wa bahari na inaweza kuweza kukaa angani kwa muda wa saa mbili.***
>
> **Mhe. Alexander Mnyeti**
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi

Baadhi wakazi wa jiji la Mwanza waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa ndege nyuki kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu, wamepongeza jitihada za serikali na kusema ni jambo la kipekee kuwa na kifaa hicho ambacho wameshuhudia namna kinavyofanya kazi kwa mara ya kwanza baada ya uzinduzi.

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka wazi kuwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki zaidi ili kuongeza wigo wa kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali nchini.



Ndege nyuki (drone) yenye namba za usajili 5H-25038 kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), ambayo ni maalum kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu ikiwa angani kwa mara ya kwanza baada ya kuzinduliwa rasmi matumizi yake na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti, katika hafla fupi iliyofanyika jijini Mwanza, ambapo ndege nyuki hiyo imegharimu zaidi ya Shilingi Milioni 259. Ndege hiyo imenunuliwa na serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. (April 13, 2025)



# Mifugo zaidi ya Milioni 370 yapatiwa Chanjo dhidi ya Magonjwa

**Na, Chiku Makwai - WMUV, Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa chanjo kwa mifugo zaidi ya Milioni 370 kwa lengo la kutibu na kuzuia magonjwa aina ya Kimeta na Homa ya Mapafu, pamoja na mifugo kukidhi matakwa ya Soko la Kimataifa.

Hayo yameelezwa Aprili 9, 2025 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa wakati akitoa Hotuba Kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bungeni jijini Dodoma.

"Kwa kuimarisha huduma za ugani na kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayovuka mipaka, katika kipindi cha Mwezi Julai, 2024 hadi Mwezi Januari 2025, serikali imenunua chanjo zenye thamani ya Shilingi Bilioni 10.1 kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini" alisema Mhe. Waziri Mkuu.

Aidha Mhe. Waziri Mkuu alisema kwa kutambua umuhimu wa ufugaji wa kisasa unaozingatia malisho bora na idadi ya mifugo inayoweza kuleta tija kwa mfugaji, serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo kwa kuwekeza ujenzi wa mabwawa manne ya Bukabwa (Butiama), Kihumbu (Bunda), Isulamilomo (Nsimbo) na Kwenkikwembe (Kilindi).

Aliongeza kuwa kutokana na Kampeni ya Tutunzane Mvomero iliyozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, uzalishaji wa mbegu za malisho umeongezeka kutoka Tani 127.8 Mwaka 2023/2024 hadi Tani 152.67 Mwaka 2024/2025 na uzalishaji wa malisho yaliyosindikwa umeongezeka kutoka Tani 728.6 hadi Tani 2,669.84.

Pia, alisema kutokana na jitihada zilizofanyika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 uzalishaji wa mifugo umeongezeka na kufikia milioni 189.8 kutoka mifugo milioni 181.8 Mwaka 2023/2024, Ongezeko hilo limechangia uzalishaji wa nyama kutoka Tani 963,856.55 kwa Mwaka 2023/2024 hadi kufikia Tani 1,054,114.03 Mwezi Februari, 2025.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuimarisha miundombinu na huduma za chanjo ya mifugo, kujenga na kukarabati minada ya mifugo, kujenga machinjio ya kisasa na kuimarisha mashamba darasa ya malisho.

Kwa Upande wa Sekta ya Uvuvi Mhe Waziri Mkuu alisema, serikali imeendelea kutekeleza mradi wa mikopo nafuu kwa wananchi ili kuwekeza katika ufugaji samaki kwa njia ya vizimba ambapo mikopo ya Shilingi Bilioni 36.64 imetolewa kwa wanufaika 7,130 kupitia mikopo hiyo, ajira 3,000 za moja kwa moja na zaidi ya 1,000 katika mnyororo wa thamani zimezalishwa.

Aliongeza kuwa serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa-Masoko na ujenzi huo utahusisha gati lenye urefu wa mita za mraba 315, jengo la utawala na vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki na kwamba ujenzi wa bandari hiyo unagharimu Shilingi Bilioni 289.5 na sasa umefikia asilimia 79 na utakapokamilika unakadiriwa kuhudumia Tani 60,000 za mazao ya uvuvi kwa mwaka na kutoa fursa za ajira takriban 30,000.

Mhe. Waziri Mkuu alihitimisha kwa kusema katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko mkoani Lindi pia kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani.

# Meli Ya Utafiti wa Uvuvi Baharini Yapokelewa Zanzibar

## Ni Meli iliyopewa jina la Dr,Fridjof Nansen kutoka nchini Norway

**Na, Hamisi Hussein - WMUV, Dodoma**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea Meli ya Utafiti wa Uvuvi kutoka Nchini Norway kwa lengo la kufanya utafiti wa wingi wa rasilimali za uvuvi na mfumo wa Ikolojia.

Akizungumzia ujio wa Meli hiyo wakati wa mapokezi yaliyofanyika Aprili 02, 2025 katika Bandari ya Malindi mjini Unguja Visiwani Zanzibar, Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu Zanzibar, Mhe. Shaaban Ali Othman alisema meli hiyo iliyopewa jina la Dr. Fridjof Nansen itaisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufahamu mwelekeo mpya wa Sekta ya Uchumi wa Buluu na kuwasaidia wavuvi kujua maeneo ambayo samaki wanapatikana kwa uhakika.

"Ujio wa meli hii kwetu sisi kama Tanzania na kama Zanzibar inatusaidia kujua uhalisia wa rasimali za uvuvi zilizomo katika bahari yetu, serikali imeshafanya uwekezaji mkubwa kupitia baharini, kwa hiyo taarifa za kitaalamu na takwimu zitakazopatikana zitawasaidia pia wavuvi wetu". alisema Mhe. Shaabani Ali Othman.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede kwa niaba ya Katibu Mkuu Prof. Riziki Shemdoe, alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kusimamia tafiti zinazofanywa na wataalamu kuhusu rasilimali za baharini ili zijikite kwenye kujua wingi wa rasilimali za uvuvi zinazopatikana kwenye bahari.

"Tutafurahi kuona utafiti uliopita ulionyesha kulikuwa na ongezeko la rasilimali tulizonazo ndani ya maji yetu lakini tunahimiza utafiti utakaofanyika awamu inayofuata Mwezi Oktoba ujikite katika kujua wingi wa rasilimali tulizonazo kwenye bahari yetu" alisema Dkt. Mhede.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), DKt. Ismael Kimirei alisema utafiti wa awamu hii umejikita kwenye maji ya Bahari ya Hindi upande wa Kusini mwa Mtwara hadi mwisho wa Pemba kwa kukusanya taarifa za wingi wa samaki, mtawanyiko wake na aina mpya za samaki zitakazopatikana.

Aidha, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) Nchini Tanzania Dkt. Nyabenyi Tipo aliwahimiza wadau kushirikiana na Serikali kufanya mijadala ya kuimarisha uhai wa viumbe maji vinavyopatikana kwenye Bahari ya Hindi ili viweze kuinua Uchumi wa Buluu na maisha ya wavuvi kwa ujumla.










# Kongamano la Nguruwe Afrika kufanyika Tanzania

***Washiriki takriban 2,000 kutoka Matifa ya Afrika kujadili fursa katika mnyororo wa thamani wa Nguruwe***

**Na, Chiku Makwai - WMUV, Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikishirikiana na Chama cha Wafugaji wa Nguruwe Tanzania (TAPIFA) imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kimataifa la Ufugaji wa Nguruwe litakalofanyika Septemba 11-13, 2025 jijini Dar es Salaam.

Hayo yamebainishwa Aprili 16, 2025 na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi uliopo katika ofisi ndogo za wizara kwenye jengo la NBC jijini Dodoma.

Mhe. Mnyeti alisema kongamano hilo linatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki takriban 2,000 kutoka mataifa mbalimbali barani Afrika wakiwemo viongozi wa serikali na wizara za kisekta, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, vijana na wanawake, wanataaluma, wadau wa maendeleo, wafugaji na wafanyabiashara katika mnyororo wa thamani wa nguruwe.

Aidha, aliongeza kuwa kongamano hilo litaambatana na mafunzo kutoka kwa wataalamu na wadau wa maendeleo katika tasnia ya nguruwe, pia washiriki kufanya majadiliano ya kibiashara na kuzitambua fursa zilizopo kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kutembelea uwandani kwa wadau kujionea namna ufugaji wa kisasa wa nguruwe unavyofanyika.

Mhe. Mnyeti alibainisha kuwa ufugaji wa nguruwe unaendana na malengo ya nchi katika kuhimiza maendeleo ya Sekta ya Mifugo ili kukuza uchumi wa nchi pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa

> *"Kongamano hilo linatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki takriban 2,000 kutoka mataifa mbalimbali barani Afrika wakiwemo viongozi wa serikali na wizara za kisekta, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, vijana na wanawake, wanataaluma, wadau wa maendeleo, wafugaji na wafanyabiashara katika mnyororo wa thamani wa nguruwe.*
>
> **Mhe. Alexander Mnyeti**
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi

# MATUKIO KATIKA PICHA

Uzinduzi wa ndege nyuki ' Drone' uliofanywa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti kwa ajili ya kudhibiti Uvuvi Haramu Ziwa Victoria Aprili 13, 2025 Jijini Mwanza.













# Prof. Shemdoe abainisha fursa za Malisho ya Mifugo

## *Aelezea jinsi Wizara inavyoajiri wataalam wa Nyanda za Malisho.*

**Na, Omary Mtamike -WMUV, Morogoro**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe amewataka wafugaji nchini kuendelea kutenga maeneo ya kuzalisha malisho ya mifugo yao ili kuboresha afya za wanyama na kujipatia kipato baada ya kuyauza.

Prof. Shemdoe alibainisha hayo Aprili 14, 2025 wakati akifungua kikao cha wataalamu wa malisho ya mifugo kilichofanyika mkoani Morogoro ambapo alitoa rai kwa vijana kuchangamkia fursa hiyo kama wanavyofanya kwenye shughuli nyingine za kiuchumi.

"Tuwawezeshe vijana waanzishe mashamba ya kulima malisho kwa sababu nina uhakika masoko yapo na nina mfano wa mtu mmoja hapa Pwani yeye kila mwaka anauza tani nyingi za malisho na hana biashara nyingine zaidi ya hiyo" alifafanua Prof. Shemdoe.

Aidha, katika hatua ya utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichopita cha wataalamu hao, Prof. Shemdoe alisema wizara yake imeendelea kuajiri vijana wengi wanaotokana na shahada ya nyanda za malisho huku pia wakiendelea kutoa elimu kuhusu chakula stahiki kwa mifugo.

Akizungumza awali kabla ya kumkaribisha Prof. Shemdoe, Mwenyekiti wa Chama cha Nyanda za Malisho ya Mifugo nchini (RST) Prof. Ismail Selemani aliishukuru Wizara kwa kufanyia kazi baadhi ya maazimio ya wataalamu hao ikiwa ni pamoja na kuboresha Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za vyakula vya Mifugo namba 180 ya Mwaka 2010 na kuendelea kutenga maeneo ya malisho na uanzishwaji wa mashamba darasa ya malisho hayo.

Akigusia fursa inayotokana na malisho Visiwani Zanzibar, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo visiwani humo Dkt. Abdultwalib Suleiman alisema kuwa wafugaji waliopo huko wamekuwa na changamoto ya uzalishaji wa malisho kutokana na sehemu kubwa ya visiwa hivyo kuzungukwa na majengo na miundombinu mbalimbali hivyo aliwataka wazalishaji wa malisho ya Mifugo kuzalisha malisho ya kutosha na kuyapeleka Zanzibar.





# Wavuvi, Wachuuzi wa Samaki Kutumia Mfumo wa "Vua, Uza na Nunua Kidigitali"

***Watu 915 wameanza kuutumia mfumo huo kipindi cha Miezi Mitatu.***

**Na, Herry Kilele - TAFIRI, Dar es Salaam**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede amewataka wavuvi, wachuuzi na wanunuzi wa samaki nchini kutumia mfumo kwa "Vua, Uza na Nunua Kidigitali (PFZ)" ili uwasaidie kuongeza ufanisi na kuboresha Sekta ya Uvuvi.

Dkt. Mhede alisema hayo Aprili 03, 2025 wakati akizindua mfumo huo katika Soko la Kimataifa la Samaki Ferry lililopo Jijini Dar es Salaam, ambapo aliwahimiza watu wote wanaouhusika na uvuaji na uuzaji wa samaki kutumia mfumo huo ambao umetajwa kutatua changamoto na kuhakikisha shughuli za uvuvi zinaleta tija kwa wavuvi na kukuza pato la Taifa.

"Mfumo huu ni hatua kubwa katika kukuza Sekta ya Uvuvi na kuhakikisha wavuvi wetu wanapata fursa bora za kibiashara ni wakati sasa wavuvi na wachuuzi wa samaki waanze kutumia mfumo huu wa PFZ," alisema Dkt. Mhede.

Katika hatua nyingine Dkt. Mhede alitaka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Zanzibar (ZAFIRI) kutoa mafunzo kwa wavuvi ili kuhakikisha kila mvuvi anafahamu namna ya kutumia mfumo huo ambapo kwa kipindi cha miezi mitatu tangu mfumo wa PFZ uzinduliwe, tayari watu 915 wamekuwa wa kitumia mfumo huo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dkt. Ismael Kimirei aliwapongeza waratibu wa Mradi wa Sapphire na kusema kuwa mradi huo ulioanza kutekelezwa Mwaka 2011 ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha Sekta ya Uvuvi inakuwa na kuchangia katika maendeleo ya Uchumi wa Buluu.

Akitoa salamu kwa wananchi Mkurugenzi wa jiji la Dar es Salaam, Mhe. Elihuruma Mabelya, alisema jiji hilo linaendelea kutoa mazingira bora kwa wavuvi na wanunuzi wa samaki, huku akipongeza TAFIRI kuanzisha mfumo huo na kueleza kuwa ni muhimu kwa wavuvi kutumia ili kuboresha biashara zao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na TAFIRI kwa uzinduzi wa mfumo huo na kuwahimiza wavuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala na maeneo mengine kutumia mfumo wa PFZ kwa ajili ya kupata mikopo itakayokuza mitaji yao.

Mhe. Mpogolo aliongeza kuwa halmashauri hiyo imejipanga kukusanya kati ya Shilingi Bilioni 140 hadi 150 katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 huku mchango wa Sekta ya Uvuvi ukitarajiwa kuwa chanzo muhimu cha mapato hayo.

# Wafugaji Wahimizwa Kupanda Malisho ya Mifugo

**Na, Stanlay Brayton - WMUV, Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Bw. Abdul Mhinte, amewataka wafugaji Wilayani Bahi na Chamwino kupanda Malisho kwa ajili ya Mifugo ili kuepukana na changamoto za kukosa malisho ya mifugo.

Akizungumza katika kikao na wafugaji cha kujadili changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi, kilichofanyika Aprili 15, 2025, Mkoani Dodoma katika Kitongoji cha Mtungutu, Kata ya Zanka, Kijiji cha Mayamaya, Wilayani Bahi, Bw. Mhinte alisema yapo maeneo muhimu ya malisho ambayo yametengwa na serikali ili kutatua changamoto za malisho.

“Yapo maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya malisho japo yanapungua kadri mifugo inavyozidi kuongezeka ni muhimu kuhakikisha kila mfugaji anapanda malisho kwa ajili ya mifugo yake.” Alisema Bw. Mhinte

Aidha, Bw. Mhite alibainisha kuwa maeneo ya malisho yanapungua kadri mifugo na watu wanavyoongezeka kiasi cha kwamba kunapelekea misitu na malisho kupungua au kutoweka kabisa.

Pia, alitoa ufafanuzi kuhusu athari za kulisha mifugo katika maeneo ya Hifadhi ya Misitu, ikiwa ni pamoja na kuharibu hifadhi hiyo na hatimaye kuhamia katika hifadhi zingine na kuziharibu na mwishowe kukosa malisho kabisa pamoja na kuharibu hifadhi hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za vyakula za Mifugo. Dkt. Asimwe Rwiguza, alisema kwa sasa serikali haitegemei malisho ya asili kwa sababu haitoshelezi idadi ya mifugo ambayo tunayo hapa nchini.

Dkt. Rwiguza alifafanua kuwa kwa sasa kuna namna ya kukabiliana na changamoto za malisho ikiwa ni pamoja na kulima malisho na ndio maana serikali imetoa maeneo maalum kwa ajili ya kupanda malisho na inaendelea kutoa mbegu hizo za malisho na kutoa elimu namna ya kupanda hizo mbegu ili kuhakikisha kila mfugaji anakuwa nazo na anapandikiza katika eneo lake.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wote, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Bw. Kusundwa Wamalwa alisema zipo changamoto nyingi zinazowakumba wafugaji wengi hususan wa Wilaya za Bahi na Chamwino, ikiwemo Maji, malisho na masoko, kwa hiyo ni vyema serikali ikaangalia namna itakavyoweza kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji hao.

Naye, Kamanda wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kati ambaye ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Bw. Mathew Kiondo alisema miaka ya nyuma TFS ilitoa Hekta 2000 kwa wafugaji ila kutokana na ongezeko la watu limepelekea mahitaji ya malisho kuwa makubwa kutokana na idadi kubwa ya watu na Mifugo.

Alifafanua kuwa TFS itaangalia namna ya kufanya ili kunasua wafugaji na changamoto ya uhaba wa maji kupitia Mfuko wa Kusaidia Jamii (CSR) ili kuwatengenezea miundombinu ya maji kutoka kwenye Hifadhi ya Msitu wa Chenene kwenda kwenye maeneo yao ya ufugaji.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Bw. Abdul Mhinte (waliokaa katikati), akiwa kwenye picha ya pamoja na wafugaji wa Wilaya za Chamwino na Bahi, baada ya kikao chake na wafugaji hao kujadili changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi, kilichofanyika Kitongoji cha Mtungutu, Kata ya Zanka, Kijiji cha Mayamaya, katika Wilaya ya Bahi, Mkoani Dodoma, Aprili 15, 2025.

# Mhinte akisisitiza Vituo vya ukusanyaji Maziwa kuongezwa

# TDB Yahimizwa Kuendelea Kusajili Wadau wa Tasnia ya Maziwa



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte, akihutubia watumishi wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), katika kikao kazi cha watumishi wa bodi hiyo, kilichofanyika katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma (Mkapa House), Aprili 16, 2025, Dodoma.

**Na. Stanlay Brayton – WMUV, Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Bw. Abdul Mhinte ameihimiza Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) kuendelea kuwatambua na kuwasajili wadau wa Tasnia ya Maziwa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini.

Bw. Mhinte alisema hayo wakati akizungumza na watumishi wa TDB katika Kikao kazi kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, Aprili 16, 2025.

"Kama wadau wa Tasnia ya Maziwa hawafahamiki na hawajasajiliwa ni ngumu sana kufikia malengo na kuzalisha maziwa kwa wingi, kwani wanahitaji kutatuliwa changamoto zao, ikiwemo za masoko ya maziwa hayo" alisema Bw. Mhinte

Vilevile, Bw. Mhinte aliongeza kuwa wadau wa Tasnia ya Maziwa wapo sehemu mbalimbali nchini ambapo ni vyema vituo vya ukusanyaji maziwa vikarekebishwa na kuongezwa ikiwa pamoja na usimamizi mzuri ili maziwa yakusanywe kwa wingi.

Bw. Mhinte ameihimiza bodi kubuni miradi mbalimbali kama maeneo ya kunywea maziwa (bar) ili kuhakikisha watumishi wanayapata kiurahisi na kuongeza Pato la Taifa.



Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Prof. George Msalya, akizungumza na Watumishi wa bodi hiyo, katika kikao kazi kilichofanyika katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma (Mkapa House), Aprili 16, 2025, Dodoma.

Naye, Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Prof. George Msalya alisema kuwa wamekuwa na kikao na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kujadili maendeleo ya bodi hususan maendeleo ya Tasnia ya Maziwa hapa nchini pamoja na utendaji kiujumla.

"Tumepokea maagizo yote tuliyopewa na Naibu Katibu Mkuu ambayo yatatujenga na kuongeza hali ya utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku katika Tasnia ya Maziwa" alisema Prof. Msalya

Halikadhalika, Prof. Msalya alisema kwa sasa maziwa yanakusanywa katika vituo 258 maalum vya kukusanyia na wataendelea kuongeza vituo vingine pamoja na miradi mingine kama Bar za Maziwa ili kuhakikisha maziwa yanapatikana kwa wingi nchini.

Prof. Msalya alibainisha kuwa kwa sasa takwimu zinaonyesha kila mtanzania anatumia takriban Lita 67.5 kwa mwaka, ila viwango vilivyowekwa kimataifa kwa mtu mmoja kunywa maziwa kwa mwaka ni Lita 200.

# Serikali Kuendelea Kuwezesha Ufugaji Wa Kisasa

## *Mhe. Mnyeti akikabidhi Mitamba 10 ya Maziwa kwa UWAMATA*

**Na. Hamisi Hussein –WMUV, Mwanza**

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kuwezesha ufugaji wa kisasa ili kuongeza tija katika uzalishaji na kukuza uchumi wa wafugaji nchini.

Hayo yameelezwa Aprili 19, 2025 na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alaxender Mnyeti wakati wa kukabidhi ng'ombe 10 wa maziwa kwa kikundi cha Umoja wa Mapadri Tanzania (UWAMATA) hafla iliyofanyika katika Shamba la Uzalishaji Mifugo lililopo Misungwi mkoani Mwanza.

Mhe. Mnyeti alisema lengo la serikali nikuona inawezesha ufugaji wa kisasa kwa kuhimiza wafugaji kuwa na mifugo michache yenye tija itakayotoa mazao bora yanayokidhi ushindani wa masoko.

"Mhe. Rais wetu anataka kuona ufugaji wa kisasa unakuwa na tija kwa wafugaji na sisi wizara tunaendelea kuhimiza ufugaji wa kisasa ambapo tumekuwa tukihamasisha ulimaji wa malisho ambayo yametajwa na wataalamu wetu kuwa yanaprotini nyingi." alisema Mhe. Mnyeti.

Kuhusu ng'ombe wa maziwa (Mitamba) waliotolewa na serikali kwa UWAMATA) Mhe. Naibu Waziri Mnyeti alisema zoezi la upandikizaji wa ng'ombe hao limefanywa na wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuwa na uhakika wa uzalishaji wa ng'ombe hao.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa UWAMATA Padri George Nzungu aliishukuru serikali kwa kuwapatia ng'ombe hao kwani wataleta tija ya uzalishaji wa maziwa na kuahidi kuwa balozi wa ufugaji wa kisasa kwa wananchi wanaozunguka eneo lao.

Aidha, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko Dkt. Yeremia Sanka alisema ng'ombe hao waliopatikana kutokana na upandikizaji wa mbegu za madume halisi ya maziwa (Friesian) na majike ya kienyeji aina ya Boran, watazalisha kati ya Lita 8 hadi 12 kwa siku tofauti na ng'ombe wa asili ambao anatoa maziwa lita 1.5 hadi 3 pekee kwa siku.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti (Katikati, Mwenye Fimbo) akiwa kwenye Picha ya Pamoja na Mapadri wa Umoja wa Mapadri Tanzania (UWAMATA) wakati wa makabidhiano ya Majike 10 ya ng'ombe wa maziwa kwenye Shamba la Uzalishaji Mifugo Mabuki, lililopo mkoani Mwanza Aprili 19, 2025.

> *Mhe. Rais wetu anataka kuona ufugaji wa kisasa unakuwa na tija kwa wafugaji na sisi wizara tunaendelea kuhimiza ufugaji wa kisasa ambapo tumekuwa tukihamasisha ulimaji wa malisho ambayo yametajwa na wataalamu wetu kuwa yana protini nyingi.*
>
> Mhe. Alexander **Mnyeti**
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi




# SERIKALI YAKABIDHI GARI LA UBARIDI KWA CHAMA CHA USHIRIKA WA UVUVI BUKASIGA

**Na, Hamisi Hussein - WMUV, Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekabidhi gari la kuhifadhia ubaridi kwa ajili ya kusafirishia mazao ya uvuvi kwa Chama cha Ushirika wa Uvuvi BUKASIGA Ltd kilichopo Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Usimamizi wa Uvuvi, Ukuzaji wa Viumbe Maji, Uchumi wa Buluu na Biashara katika Ukanda wa SADC (PROFISHBLUE).

Akikabidhi gari hilo kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Aprili 30, 2025 katika ofisi za wizara zilizopo kwenye Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede alisema serikali inaendelea kuwawezesha wananchi wanaojihusisha na mnyororo wa thamani wa Sekta ya Uvuvi kikiwemo Chama cha Ushirika wa Uvuvi BUKASIGA.

“Serikali imetumia rasilimali zake kuhakikisha BUKASIGA Ltd inasimama, ndiyo ilisaidiwa na serikali wakati wa kuingia kwenye mchakato shindani wa mradi wa PROFISHBLUE ambao unatumia fedha za serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB) mradi unaolenga kuongeza ubora wa mazao na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi, kwahiyo gari hili likafanye kazi iliyokusudiwa na likasafirishe samaki tu.” alisema Dkt. Mhede.

Aidha, Dkt. Mhede alimuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi Dkt. Baraka Sekadende kukisaidia chama hicho kufanya usajili wa gari hilo pamoja na kuliwekea chapa ’branding’ zitakazoonesha usafirishaji wa mazao ya samaki ili lisitumike kwa matumizi mengine.

Kwa upande wake Dkt. Sekadende akizungumza kwenye hafla hiyo alisema kuanzia Mwaka 2019 wizara imefanikiwa kuanzisha vyama vinne vya ushirika wa uvuvi kikiwemo cha BUKASIGA Ltd ambacho ndicho kimekabidhiwa gari hilo litakalopunguza upotevu wa mazao ya uvuvi.

Naye Mwakilishi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ambaye ni Mrajisi wa Ushirika mkoani humo Bi. Hilda Boniface alishukuru jitihada zinazofanywa na serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuvisaidia vyama vya ushirika kukua kupitia Sekta ya Uvuvi na kutoa wito kwa vyama vyote vya ushirika kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali, huku Mwenyekiti wa BUKASIGA Ltd Bw. Erasto Majura akiishukuru Serikali na kuahidi kulisimamia gari hilo liweze kuwanufaisha wanachama na jamii kwa ujumla.

Gari la kuhifadhia ubaridi lililokabidhiwa kwa Chama cha Ushirika wa Uvuvi cha BUKASIGA Ltd lina thamani ya Dola za Kimarekani 87,230.99.

# MATUKIO KATIKA PICHA

**Timu ya Viongozi na watalaamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Riziki Shemdoe na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Aprili 25, 2025 imefika na kukagua eneo la Nyakabindi kunakotarajiwa kufanyika hafla ya uzinduzi wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo za Mifugo.**









# MATUKIO KATIKA PICHA

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti alivyowakabidhi Mapadri wa Umoja wa Mapadri Tanzania (UWAMATA) Majike 10 ya ng'ombe wa maziwa yenye mimba (mitamba) kwenye Shamba la Uzalishaji Mifugo Mabuki, mkoani Mwanza Aprili 19, 2025.**











# MATUKIO KWENYE PICHA

Shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Viongozi na Wataalamu wa Wizara ya mifugo na uvuvi katika kipindi cha Mwezi Machi Mwaka 2025 katika maeneo mbalimbali nchini.














# MATUKIO KWENYE PICHA

Shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Viongozi na Wataalamu wa Wizara ya mifugo na uvuvi katika kipindi cha Mwezi Machi Mwaka 2025 katika maeneo mbalimbali nchini.







Baadhi ya Wataalam wa Idara ya Huduma za Mifugo nchini kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Mkurugenzi wa idara hiyo Dkt. Benezeth Lutege walivyotoa elimu ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kupitia vyombo vya habari kuanzia Aprili 08 - 11, 2025 kuelekea Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo za Mifugo na Utambuzi mwaka huu.










# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

Wizara ya Mifugo na Uvuvi